JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
JESHI LA POLISI TANZANIA

Anwani ya Simu: "MKUUPOLISI"
SimuNambari:0262323585
Fax.Na.02623L23586

Unapojibu tafadhali taja

Ofisi ya
Mkuu wa Jeshi la Polisi,
Makao Makuu ya Polisi,
4 Mtaa wa Posta,
S.L.P. 961,
40483 DODOMA

Kumb: **GA/PF/ E.2716/88**

18 Januari, 2024

Kwa: E.2716 SSGT FRANCIS GERALD LUWANGA

K. K. Kamanda wa Polisi,
Mkoa wa Temeke,
S.L.P 9140
DAR ES SALAAM.

YAH:**KUSTAAFU KAZI KWA UMRI WA LAZIMA**

Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.

2. Taarifa zako za kiutumishi zinakinzana kuhusu tarehe yako ya kuzaliwa **NIDA** inaonyesha ulizaliwa tarehe **12/12/1969**, na **PF. 104 A** inaonyesha ulizaliwa tarehe **01/07/1969** na **HCMIS** inaonyesha ulizaliwa tarehe **01/07/1969.**
3. Waraka wa Utumishi wa Umma **Na.1wa mwaka 2018** aya ya **4.22**. Kanuni **F.47(2)** unaeleza utaratibu wa kutambua tarehe ya kuzaliwa kwa Mtumishi wa Umma ambaye kuna taarifa zaidi ya moja zinazokinzana kuhusu tarehe yake ya kuzaliwa kwamba **taarifa yoyote rasmi inayobainisha umri mkubwa zaidi wa mtumishi husika ndiyo itahesabika kuwa inabainisha umri sahihi wa Mtumishi.**
4. **HCMIS na PF 10-4 A** zinaonesha ulizaliwa tarehe **01/07/1969** ndiyo zinakupa umri mkubwa zaidi hivyo utafikisha umri wa miaka **55** ifikapo tarehe **01/07/2024**. Kwa cheo ulichonacho cha **Stafu Sajini** kustaafu kwako kazi kwa umri wa lazima wa miaka **55** ni tarehe **01/07/2024**.
5. Umepewa likizo ya siku **28** kuanzia tarehe **03/06/2023** hadi **30/06/2024.** Kabla ya kupewa hati ya kustaafu (Discharge Certificate) kabidhi kitambulisho, sare na vifaa vya Serikali kwa mkuu wa Polisi Wilaya/kikosi. Nenda katika Ofisi za **PSSSF** zilizoko Makao Makuu ya Mkoa kuthibitisha usajili cheki. Na..**8166339** Endapo hukusajiliwa jaza kikamilifu fomu **PSSSF**.

CamScanner

6. Omba msafao ya kustaafu kwa kujaza fomu Ben 1 nakala mbili halisi. Fomu hizo zijazwe kikamilifu na zibandikwe picha na zitumwe zote makao makuu ya polisi zikiwa na nyaraka za vivuli vifuatavyo:- **Barua ya ajira,kibali cha kustaafu kazi, barua ya cheo cha mwisho, barua ya kuthibitishwa kazini, hati ya mshahara ya hivi karibuni (Salary Slip) visibitishwe na mwajiri. Kitambulisho cha Taifa/Mpiga Kura/Leseni ya udereva kithibitishwe na mwanasheria au mahakamani na taarifa fupi ya benki anayopokelea mshahara** kwa ajili ya kushughulikia mafao. Mshahara wako utafutwa tarehe **01/07/2024.**

7. Mkuu wa Jeshi la Polisi anakushukuru na kukupongeza kwa kazi nzuri ulioifanya kwa muda wote uliolitumikia Jeshi la Polisi na Taifa kwa ujumla.Mwisho anakutakia kila la kheri wewe na familia yako katika maisha yako mapya nje ya Jeshi.

Wankyo R. Nyigesa - ACP
Kny: MKUU WA JESHI LA POLISI

Kny: MKUU WA JESHI LA POLISI

Nakala: Katibu Mkuu,
Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi,
Mji wa Serikali – Mtumba,
Mtaa wa Habari/Afya,
S.L.P 2916,
DODOMA. - Kwa taarifa

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais,
Menejimenti ya Utumisi wa Umma,
Mji wa Serikali,
Mtumba Mtaa wa Utumishi,
S.L.P 670,
DODOMA. - Kwa taarifa

Mkurugenzi Mkuu,
Mfuko wa Pensheni **PSSSF**,
DODOMA. – Kwa taarifa

CO PAYROL - Mfute kwenye orodha mishahara na posho ifikapo tarehe **01/07/2024.**

CO C&B - Muandalie fomu kwa ajili ya kuombea mafao

CamScanner